# TADB wahamasisha ufugaji ng'ombe wa maziwa

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

KIWANDA cha kuchakata maziwa cha Jijini Tanga cha Tanga Fresh kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa maziwa kutoka kwa wafugaji hatua iliyosababisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kuwafaka wafugaji wa ng'ombe kuchangamkia fursa hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana mkoani hapa Mtendaji Mkuu wa kiwanda hicho, Innocent Mushi, wakati akitoa maelezo kwa ujumbe wa Benki wa TADB. Mushi aliishukuru TABD kwa kuiwezesha kujenga miundombinu ya kisasa ya kupokea maziwa inayokiwezesha kupokea maziwa yakiwa safi na salama. Ujumbe wa TADB uliongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Japhet Justine.

"Tumejenga vituo vya kisasa ili kurahisisha ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa wafugaji wa maeneo mbali mbali katika jiji la Tanga. Miundombinu hii inasaidia kupunguza upotevu wa maziwa au kuharibika njiani kwani wengi wafugai wanatoka maeneo ya mbali na kiwanda kilipo," alisema Mushi.

Kiongozi huyo alisema Tanga Fresh tayari imenufaisha zaidi ya wafugaji 6,000 kwa kununua maziwa yao katika maeneo mbali mbali mkoani Tanga na mikoa ya jirani ya Kilimanjaro na Arusha na pia mikoa mingine ya Morogoro, Mbeya na Njombe.

Justine aliuomba Mkoa wa Tanga kuongeza idadi ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa sababu Tanga Fresh ni soko kubwa la maziwa kwa wafugaji wa Mkoa wa Tanga na mikoa mingine.

"TADB imekopesha vyama viwili vya ushirika ya wafugaji na vinasambaza maziwa kwa wananchi na kukiuzia maziwa Tanga Fresh. Tumo mbioni kuviwesesha vyama 26 ili kuboresha mnyororo wa thamani wa malighafi hii na kuinua mapato ya wafugaji mkoani humu," alisema Justine.

Aliwaomba wafugaji kuanzisha vyama vya msingi vya ushirika ili waweze kupata mikopo ya masharti nafuu kutoka TADB na benki za CRDB, NMB, StanicBank.

"Kiwanda hiki ni soko la uhakika kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa nchini na kina uhitaji mkubwa wa maziwa kuliko maziwa yanayozalishwa. Nawaomba wafungaji wajiunge katika vyama vya msingi, wakopesheke, ili waweze kuboresha mifugo yao na kuchochea uzalishaji wa maziwa kwa wingi," alisema Justine.

Justine alisifu ujenzi wa vituo vya kupokea maziwa Jijini Tanga na kusema miundombinu hiyo ni hatua mihimu katika kuinua mnyoyoro wa thamani wa malighafi ya kiwanda hicho. "Ujenzi wa vituo hivi utasaidia upatikanaji wa malighafi hiyo kwa urahisi na kwa ubora unaotakiwa ili hata bidhaa zitakazozalishwa ziwe na bora unaotakiwa sokoni," alisema Justinena kuwaomba wafugaji wachangamkie furusa hiyo.

Alisema viwanda vya maziwa vya Tanzania vina uwezo kuwa kuchakata lita 150,000 za maziwa kwa siku, lakini havipati maziwa ya kutosha. Aliwasihi wafungaji kuungana katika vyama vya ushirika ili waboreshe mifugo yao na itoe maziwea kiwa wingi na yenye ubora unaokubalika. Alisema TADB na benki washirika za CRDB, NMB, na StanbicBank na taasisi nyingine za kifedha zinafanya juhudi kiwawezesha wazalishaji katika sekta za kilimo, uvuvi,na ufugaji kuzalisha mazao bora na kuinua vipato vyao.



Mgombea Ubunge Jimbo la Kisesa, Luhaga Mpina, akihakiki nyaraka muhimu kabla ya kurejesha fomu ya kuomba kuteuliwa na Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) kwa ajili ya kugombea nafasi hiyo. Wengine ni Katibu wa CCM Wilaya ya Meatu, Charles Mazuri na mwenyekiti wa CCM wilayani humo Juma Mwiburi. (Na Mpigapicha Wetu)

# Wazashaji bidhaa za alizeti, ubuyu watoa kilio serikalini

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA ya viwanda nchini imeiomba Serikali kuharakisha utekelezaji wa mchakato wa kuanzisha bodi ya mafuta ya alizeti.

Ombi hilo limetolewa jijini Dodoma jana na baadhi ya wamiliki wa viwanda vya alizeti na ubuyu walipokuwa wakizungumza na Majira kuhusiana na changamoto wanazokabiliana nazo.

Mmoja wa wamiliki wa viwanda hivyo, Jackson Masawe, alisema ombi kuu kwa Serikali ni kuanzishwa bodi ya mafuta ya alizeti ili kuiwezesha sekta hiyo kuingia vizuri kwenye uchumi wa kati.

Maswe ambaye ni mmiliki wa kiwanda cha mafuta ya alizeti cha JACKMA J Enterprises, alisema baadhi ya wamiliki wa viwanda hivyo, waliotoa changamoto wanazokumbana nazo kwa wizara ya viwanda na biashara, kwa mrefu lakini utekelezaji bado ni mdogo.

INAENDELEA UK. 7

Scanned with CamScanner

Waandishi wa habari, kina wajibu wa kutoa mafunzo kwa Alisema waandishi wa habari lazima watende haki na kuripoti ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania, Kajubi Mkangaja.




**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wadau wa uvuvi muda mfupi baada ya kufungua mkutano wa wadau kuhusu mjadala wa viwango vya mazao ya dagaa na mwani, uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi (WMUV), Ezra Mutagwaba (kushoto) Mratibu wa Mradi wa SWIOFish, Daniel Nkondola.** (Na Mpigapicha Wetu)

# Serikali kutengeneza viwango vya ubora wa dagaa, mwani

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema ipo katika mchakato wa kutengeneza viwango vya kitaifa vya ubora na usalama wa mazao ya mwani na dagaa, ili kuyapa mazao hayo fursa pana ya masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah alipokuwa akifungua mkutano wa wadau kuhusu mjadala wa viwango vya mazao ya dagaa na mwani uliofanyika juzi jijini Dar es Salaam.

Dkt. Tamatamah alisema, kutengenezwa na kuanzishwa kwa viwango vya kitaifa vya ubora na usalama wa mazao hayo ya uvuvi, kutaimarisha na kukuza soko la kitaifa na kimataifa la bidhaa zinazotokana na mazao hayo ya uvuvi.

"Mazao ya dagaa na mwani kwa muda mrefu, yamekuwa hayana viwango vya ubora jambo ambalo limekuwa likifanya bidhaa hizo, kutokutambulika katika soko la kimataifa ndiyo maana sasa serikali imeamua kutengeneza viwango vya ubora vya mazao ya uvuvi, hasa daagaa na mwani ili yaweze kupata masoko yenye uhakika ndani na nje ya nchi," alisema Dkt. Tamatamah.

Alisema uvuvi wa dagaa pamoja na ukulima wa mwani ni muhimu kwa uchumi wa jamii inayoishi Pwani na taifa kwa ujumla, huku akisema kilimo cha mwani peke yake kinawahusisha takribani wakulima 3,000 wengi wao wakiwa ni wanawake.

Dkt. Tamatamah alisema, kutokana na umuhimu huo ni dhahiri kwamba kuna haja ya kuwepo kwa viwango vya ubora na usalama, ili wafanyabiashara waweze kuyafikia masoko mbalimbali duniani.

Naye Mkulima wa mwani wilayani Bagamoyo, Machao Jingalao alisema hatua hiyo ya serikali ya kutengeneza viwango vya ubora kwa ajili ya mazao hayo ya uvuvi ni hatua nzuri ya kuelekea uchumi wa viwanda.

"Naiomba serikali iongeze nguvu katika kuimarisha biashara hii ya mazao ya uvuvi, kwani ikisimamiwa vizuri itasaidia kuiongezea mapato nchini na kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja," alisema Jingalao.

Khimji ali
wakati akizu
wa habari n
kurejesha f
nafasi hiyo
wa Kata ya
Alisema
kutekeleza
asilimia 99
kero mbali
wananchi
Alitaja ba
alizozipatia
uongozi w
wa shule,
ya wanafu
kidato cha
ya kusoma
Diwani mv
kujenga sh
ikiwemo S
Mivinjeni.
"Shule y
ina kidato
tatu, ina u
watoto 50
Sekondari
imeanza k
hadi sasa,
Shule ya S
wanafunzi
Mgomb
wakati alip
Kamati ya
amefanikiv
mbalimbal
kupitia fed
halmashur
ajili ya kuw
vijana na w
Pia aliser
wake kama
na usalama
na kuhakiki
uhalifu yana
yote ya kat
Aliongez
pia, kuhaki
safi na sala
kuwaondo
waliyokua
nyuma.
Hata h
kampeni
kuwatak
kunadi s
wa kuw
kutatua
maendo

Scanned with CamScanner



Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa (wa tatu kulia), akikata utepe kuzindua tawi la benki ya NMB Mlimba wilayani Kilombero, mkoani Morogoro jana. Kushoto ni Meneja wa benki hiyo, Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, Meneja wa tawi la NMB Mlimba, Omary Mtibiro na Kaimu Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Salie Mlay. Habari Uk. 9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

NIPASHE UK 8.

# *TADB yahamasisha ufugaji ng'ombe wa maziwa*

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imehamasisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kukabiliana na upungufu wa bidhaa hiyo katika kiwanda cha kuchakata maziwa cha jijini Tanga.

Kiwanda hicho kinakabiliwa na upungufu wa maziwa kutoka kwa wafugaji.

Hayo yalibainishwa na Mtendaji Mkuu wa kiwanda hicho, Innocent Mushi jana alipokuwa akitoa maelezo kwa ujumbe wa TADB ulioongozwa na na Mkurugenzi Mtendaji, Japhet Justine.

Hata hivyo, Mushi aliishukuru TADB kwa kuiwezesha kujenga miundombinu ya kisasa ya kupokea maziwa inayokiwezesha kupokea maziwa yakiwa safi na salama.

"Tumejenga vituo vya kisasa ili kurahisisha ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa wafugaji wa maeneo mbalimbali katika jiji la Tanga. Miundombinu hii inasaidia kupunguza upotevu wa maziwa au kuharibika njiani kwani wengi wafugai wanatoka maeneo ya mbali na kiwanda kilipo," alieleza Mushi.

Alisema Tanga Fresh imenufaisha zaidi ya wafugaji 6,000 kwa kununua maziwa yao katika maeneo mbalimbali mkoani Tanga na mikoa ya jirani ya Kilimanjaro na Arusha na pia mikoa mingine ya Morogoro, Mbeya na Njombe.

Justine aliuomba Mkoa wa Tanga kuongeza idadi ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa sababu Tanga Fresh ni soko kubwa la maziwa kwa wafugaji wa Mkoa wa Tanga na mikoa mingine.

"TADB imekopesha vyama viwili vya ushirika ya wafugaji na vinasambaza maziwa kwa wananchi na kukiuzia maziwa Tanga Fresh. Tumo mbioni kuviwezesha vyama 26 ili kuboresha mnyororo wa thamani wa malighafi hii na kuinua mapato ya wafugaji mkoani humu," alisema Justine.

Aliwaomba wafugaj kuunda vyama vya msingi vya ushirika ili waweze kupata mikopo ya masharti nafuu kutoka TADB na benki za CRDB, NMB, StanicBank.

Bw Justine alisifia ujenzi wa vituo vya kupokea maziwa Jijijni Tanga na kusema miundombinu hiyo ni hatua muhimu katika kuinua mnyoyoro wa thamani wa malighafi ya kiwanda hicho.

"Ujenzi wa vituo hivi utasaidia upatikanaji wa malighafi hiyo kwa urahisi na kwa ubora unaotakiwa ili hata bidhaa zitakazozalishwa ziwe na bora unaotakiwa sokoni," alisema.

Alisema viwanda vya maziwa vya Tanzania vina uwezo kuwa kuchakata lita 150,000 za maziwa kwa siku, lakini havipati maziwa ya kutosha.

Mamlaka ya ...
vya ndege vya Zanzibar
kulizungushia uzio eneo

*HABARI LEO UK 19.*

# TADB yahamasisha ufugaji ng'ombe wa maziwa

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

TANGA Fresh, kiwanda cha kuchakata maziwa cha Jijini Tanga, kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa maziwa kutoka kwa wafugaji, Mtendaji Mkuu wa kiwanda hicho, Innocent Mushi ameeleza hapa jana.

Akitoa maelezo kwa ujumbe wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Mushi ameishukuru TABD kwa kuiwezesha kujenga miundombinu ya kisasa ya kupokea maziwa inayokiwezesha kupokea maziwa yakiwa safi na salama.

Ujumbe wa TADB umeongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Japhet Justine.

"Tumejenga vituo vya kisasa ili kurahisisha ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa wafugaji wa maeneo mbali mbali katika jiji la Tanga. Miundombinu hii inasaidia kupunguza upotevu wa maziwa au kuharibika njiani kwani wengi wafugaji wanatoka maeneo ya mbali na kiwanda kilipo," alisema Mushi.

MTANZANIA UK 18.

# Mwani, dagaa kuwekewa viwango vya ubora

Na MWANDISHI WETU
-DAR ES SALAAM

SERIKALI imesema ipo katika mchakato wa kutengeneza viwango vya kitaifa vya ubora na usalama wa mazao ya mwani na Dagaa ili kuyapa mazao hayo fursa pana ya masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah alipofungua mkutano wa wadau kuhusu mjadala wa viwango vya mazao hayo uliofanyika Dar es Salaam juzi.

Alisema kutengenezwa na kuanzishwa kwa viwango vya kitaifa vya ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kutaimarisha na kukuza soko la kitaifa na kimataifa la bidhaa zinazotokana na mazao hayo ya uvuvi.

"Mazao ya dagaa na mwani kwa muda mrefu yamekuwa hayana viwango vya ubora, jambo ambalo limekuwa likifanya bidhaa hizo kutokutambulika katika soko la kimataifa, ndiyo maana sasa Serikali imeamua kutengeneza viwango vya ubora vya mazao ya uvuvi hasa dagaa na mwani ili kupata masoko yenye uhakika ndani na nje ya nchi,"alisema.

Alisema uvuvi wa dagaa na ukulima wa mwani, ni muhimu kwa uchumi wa jamii inayoishi Pwani na taifa kwa ujumla, huku akisema kilimo cha mwani peke yake kinawahusisha takribani wakulima 3,000, wengi wao wakiwa ni wanawake.

"Kwa mwaka 2019/20 kiasi cha tani 1,449 za mwani zilizalishwa na kati ya hizo, asilimia 10 zilitumika hapa nchini kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwemo sabuni na asilimia 90 zilisafirishwa kwenda nje ya nchi zikiwemo nchi za China, Marekani, Canada, Uingereza, Denmark na Ufaransa.

"Zanzibar uzalishaji wa mwani umefikia takriban tani 35,000,ndiyo bidhaa ya pili inayosafirishwa kwa wingi kwenda nje ya nchi,"alisema.

Alisema kutokana na umuhimu huo, ni dhahiri kuna haja ya kuwapo viwango vya ubora na usalama ili wafanyabiashara waweze kuyafikia masoko mbalimbali duniani.

Mkulima wa Mwani, wilayani Bagamoyo, Machao Jingalao alisema hatua ya Serikali ya kutengeneza viwango vya ubora kwa ajili ya mazao hayo ya uvuvi ni hatua nzuri ya kuelekea uchumi wa viwanda.

- PICHA:MPIGAPICHA WETU

